KY Standards

Your home for Kentucky Academic Standards.

# Karibu kwenye Darasa la 3!

## Mwongozo wa Familia kwa *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky*

Mwongozo huu uliundwa ili kusaidia familia kuelewa *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* na kuonyesha kile ambacho watoto watajifunza kufikia mwisho wa darasa la 3. Ala hii inatoa taarifa kuhusu mawazo na mastadi muhimu ambazo walimu wataanzisha katika hesabu, kusoma na kuandika, sayansi na masomo ya kijamii. Inajumuisha mifano inayowezekana ya kile wanafunzi wataombwa kufanya darasani, jinsi ya kumsaidia mtoto wako nyumbani, maswali unayoweza kumuuliza mwanafunzi wako wa darasa la 3 na maswali ambayo familia zinaweza kumuuliza mwalimu wa mtoto wao.

Mwongozo huu pia uliundwa ili kuwasaidia wazazi kuelewa jinsi wanavyoweza kufanya kazi na walimu kusaidia majifunzo ya mwanafunzi wao wa darasa la 3. Walimu na familia wanapofanya kazi pamoja ili kuwasaidia wanafunzi kufahamu *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky*, wanafunzi wanaweza kufaulu kwa kukuza ujuzi watakaohitaji maishani baada ya kuhitimu.

Ikiwa una maswali kuhusu maelezo haya au ikiwa mtoto wako anahitaji usaidizi wa ziada, tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako.

### Kwa nini Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky ni Muhimu?

*Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* ni muhimu kwa sababu yanasaidia kuhakiksha kwamba wanafunzi wote, haidhuru wanaishi wapi au wanasoma shule gani, wana ujuzi wanaohitaji ili kupata maisha bora ya baadaye. Viwango vinawakilisha lengo au matokeo ya eneo la somo (kama vile hesabu, kusoma na kuandika, sayansi na masomo ya kijamii). Zinasaidia kuweka matarajio ya wazi na thabiti kwa kile ambacho wanafunzi wanapaswa kujua na kuweza kufanya kuanzia shule ya chekechea hadi shule ya sekondari. Viwango ni mtaala na havibainshi muundo wa mpango wa somo au jinsi vitengo vinapaswa kupangwa. Maamuzi ya jinsi bora ya kuwasaidia wanafunzi kufikia malengo katika viwango yanaachiwa wilaya za shule za mitaa na walimu.

### Viwango vimepangwa vipi?

*Viwango vya Kitaaluma vya* Kentucky vimepangwa tofauti kulinagna na eneo la maudhui. Baadhi ya *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* yamepangwa darasa kwa darasa, pale nyingine zikiwekwa katika viwango kadhaa vya darasa, kama vile "shule ya sekondari" kwa darasa la 9-12. Katika masomo yote, viwango vinaonyesha kile ambacho wanafunzi wanapaswa kujifunza na kuweza kufanya, lakini si jinsi uzoefu huo wa kujifunza unapaswa kutengenezwa au ninyenzo gani zinafaa kutumia. Kwa maelezo zaidi kuhusu *Viwango vya Kitaaluma vya Kentucky* , tembelea https://kystandards.org/ ili kusoma viwango kamili na kupata nyenzo zinazohusiana na viwango..

KYstandards.org
standards@education.ky.gov
facebook.com/kydeptofed
@KyDeptofEd

# Hesabu Katika Darasa la 3

## Muhtasari:

Wakati wa darasa la 3,wanafunzi watakuza uwezo wa kuzidisha na kugawanya hadi 100 na kujumlisha na kutoa hadi 1,000 kwa kutumia thamani ya mahali na sifa za uendeleshaji. Mtoto wako ata::

- Wakilisha na kutatua matatizo kwa kutumia kuzidisha na kugawanya;
- Kuwa na uzoefu wa aina mbalimbali ya sehemu za kujiandaa kwa darasa la 4.;
- Tumia duru ili kukadiria majibu kwa matatizo ya kujumlisha na kutoa ili kuamua kama jibu lina maana;
- Tatua matatizo yanayohusisha kipimo; na
- Elewa na kutumia mchakato wa takwimu.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni::

Kutumia thamani ya mahali kuzungusha namba hadi 10 au 100 iliyo karibu zaidi;
Kuzidisha na kugawanya hadi 10 x 10;
Kuweka sehemu kwenye mstari wa namba pamoja na namba nzima;
Kulinganisha sehemu kwa kutumia michoro;
Kuwaambia na kuandika muda kwa dakika;
Kutatua matatizo ya wakati uliopita;
Kutambua swali la takwimu, kukusanya data na kuunda chati au grafu ili kufanya uchunguzi kuhusu data; na
Kuainisha maumbo kwa idadi ya pande na pembe.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

Cheza michezo ya hesabu na mtoto wako kama vile: Ni namba gani mbili ambazo zinaweza kukupa jibu kati ya 30 na 40? Je! unaweza kufikiria namba zingine ambazo zinaweza kufanya kazi?
Chunguza sehemu ndogo jikoni. Uliza maswali kama vile: Je, 1/3 vikombe ngapi tungehitaji kutengeneza kikombe kizima? 1/4 vikombe vingapi kwenye kikombe 3/4?

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

Je, sehemu zikoje kama namba zingine?
Je, tunawezaje kuweka kadi zetu za mchezo ili kuwe na namba sawa katika kila safu?
Ni ipi baadhi ya mifano ya ulimwengu halisi ya vitu vinavyokuja kwa makundi sawa? (Kwa mfano, pakiti za ubani/chingamu [chewing gum], masanduku ya juisi, pakiti za penseli).

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako:

Je, mtoto wangu anaitikiaje kazi ngumu darasani?
Ni hatua gani ya kwanza ambayo mtoto wangu anachukua ili kutatua tatizo la ulimwengu halisi?
Ni mikakati gani ya kuzidisha na kugawanya inafanya kazi vizuri kwa mtoto wangu?
Unafikiri ni nini kinampa mtoto wangu shida zaidi? Je, ninaweza kumsaidiaje kuboresha?
Ninawezaje kusaidia ukuaji wa mtoto wangu katika hesabu?

# Kusoma na Kuandika Katika Darasa la 3

## Muhtasari:

Wakati wa darasa la 3, wanafunzi watasoma kwa ufasaha na kwa kujieleza, na pia kufanya mazoezi ya mikakati mbalimbali ya kusoma na kuandika kwa kujiamini. Mtoto wako ata:

- Tumia mikakati tofauti kusoma maneno yasiyojulikana ambayo yana silabi nyingi;
- Sikiliza, soma, zungumza na andika kuhusu hadithi za kubuni na zisizo za kubuni za darasa la 3 kwa kutumia vidokezo kutoka maandishi ili kusaidia kuleta maana kuchambua walichosoma;
- Unda herufi zote za kubwa na ndogo kwa mkono ili kutoa maneno na sentensi zilizoandikwa kwa mkono zinazoweza kusomeka; na
- Ongea na kuandika ipasavyo kwa kutumia sehemu za hotuba, herufi kubwa, vituo, na mifumo ya tahajia ya jumla, pamoja na lugha inayoonyesha msamiati unaokua; tumia faharasa/kamusi za mwanzo.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni::

Kubainisha na kueleza jinsi maandishi yalivyoundwa, ikijumuisha ulinganisho, sababu/athari na miundo ya tatizo/suluhisho;
Andika maoni juu ya mada au maandishi yenye ushahidi na sababu zinazounga mkono, kwa kutumia teknolojia, inapofaa;
Kuunda herufi zinazosomeka, maneno na sentensi; na
Kubainisha au kufafanua maana ya maneno na vishazi visivyojulikana na vyenye maana nyingi.

## Jinsi Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani::

Chagua shairi, wimbo au hadithi fupi katika kiwango cha kusoma cha mtoto wako (muulize mwalimu wa mtoto wako ni kiwango gani cha kusoma kinachomfaa zaidi) na ujizoeze kusoma (au kuimba) kwa sauti tena na tena.
Chagua vitu viwili au vitatu karibu na nyumba yako. Mwambie mtoto wako afikirie na aeleze jinsi vitu vinavyofanana na tofauti kutoka kwa kila mmoja.
Toa maoni kuhusu mada au suala na toa sababu za kuunga mkono maoni hayo.
Andika orodha ya mboga au orodha ya matakwa kwa mkono.
Mhimize mtoto wako kuuliza maneno mapya yanamaanisha nin

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

Unasoma nini darasani? Unaweza kuniambia nini kuhusu hilo?
Je, unaweza kuunganishwa na kile kinachotokea katika maandishi? Kwa ninini hivyo au si hivyo?
Umejifunza nini kutokana na maandiko? (Kumbuka, maandishi yanaweza kuwa chochote kinachowasilisha ujumbe, kwa hivyo mafunzo yanaweza kutoka kwa kumsikiliza mtangazaji, kutazama video au kusoma ubao wa matangazo, kwa mfano.)
Je, unaweza kunionyesha sampuli ya kitu ambacho umeandika hivi majuzi? Niambie jinsi ulivyoamua utakachoandika. Nionyeshe sehemu ya uandishi wako ambao unajivunia/bado unafanyia kazi/ungependa kuboresha zaidi.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako::

Mtoto wangu anasoma na kuandika nini shuleni, na ni mada gani zinazochunguzwa?
Mtoto wangu anahitaji kujifunza maneno gani ya msamiati?

Ninawezaje kuhimiza kujifunza nyumbani na ni nyenzo gani ninahitaji ili kumsaidia mtoto wangu?

# Sayansi Katika Darasa la 3

## Muhtasari:

Wakati wa darasa la 3, mtoto wako atajifunza ujuzi unaokuza uchanganuzi na ufasiri wa data, fikra makini, utatuzi wa matatizo na miunganisho katika maeneo mbalimbali ya sayansi. Mtoto wako ata:

- Angalia data na hali ya hewa inayotarajiwa wakati wa majira fulani. Watatumia taarifa hii kuja na suluhu za kupunguza athari za hali ya hewa kali;
- Angalia mizunguko mbalimbali ya maisha na kuelewa kwamba viumbe vina sifa tofauti, baadhi ni za kurithi na baadhi zinazoathiriwa na mazingira;
- Tumia sumaku kuangalia uhusiano wa sababu -na- athari na nguvu; na
- Zingatia kanuni za usanifu wa uhandishi ili kutatua matatizo, kama vile kwa nini baadhi ya madaraja hustamihili nguvu za asili, huku nyingine zikiporomoka.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni::

Kuchunguza jinsi majengo yameundwa kustahimili tufani na vimbunga;
Kwa kutumia modeli za mizunguko ya maisha kueleza kwamba viumbe mbalimbali vina kuzaliwa, kukua, kuzaliana na kifo kwa pamoja;
Kulinganisha jinsi wanyama wanavyoishi katika mazingira yao; na
Kufanya majaribio ili kuona jinsi nguvu inavyoathiri nguvu na mwelekeo wa mwendo.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani:

Fuatilia halijoto na mvua wakati wa majira ya joto, majira ya majani kupukutika, majira ya baridi, na majira ya kuchipua ili kutafuta ruwaza.
Unapotazama filamu au kusoma vitabu vilivyowekwa katika majimbo au nchi nyingine, msaidie mtoto wako kutambua mfanano na tofauti za hali ya hewa.
Toa aina mbalimbali za sumaku ili mtoto wako atumie kuchunguza.
Shiriki katika programu za ulimwenguni katika jamii.
Tembelea mbuga za wanyama na mbuga za jimbo/taifa na tumia njia za kupanda mlima, baiskeli na njia ya kukatambuga ili kuona vikundi vya wanyama na kujadili jinsi kikundi kinavyofanya kazi pamoja ili kusaidia washiriki wote kuishi.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

Je, hali ya hewa ya Kentucky ni tofauti vipi wakati wa majira ya joto kuliko wakati wa majira ya baridi?
Je, hali ya hewa ya Kentucky ni tofauti vipi na hali ya hewa huko Alaska? Texas?
Je, umerithi sifa gani?
Nini kinatokea kwa wanyama tunapofyeka magugu ili kujenga nyumba?
Wakati wa kuvuta kamba, ni nini yatokea pande zote mbili zikivutana kwa nguvu sawa? Nguvu tofauti?
Je, ukubwa wa sumaku unaifanya kuwa na nguvu au dhaifu?

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako:

Je, ni nyenzo gani ninazoweza kutumia kumsaidia mtoto wangu nyumbani?
Tunapaswa kurekodi vipi uchunguzi wetu wa hali ya hewa?

Ni njia gani tofauti za kujadili nguvu na mtoto wangu?
Je, ni programu gani za jamii unazojua ambazo zinaweza kuimarisha sayansi anayojifunza?

# Masomo ya Kijamii Katika Darasa la 3

## Muhtasari:

Katika darasa la 3, wanafunzi watatumia wazo la jamii duniani kote, kuelewa athari ya uhusiano wa binadamu kati ya makundi katika mabara/kontinenti tofauti. Mtoto wako ata:

- Eleza madhumuni ya kimsingi na kazi za mabaraza mbalimbali ya uongozi duniani huku ukilinganisha jinsi jamii mbalimbali zinavyojitawala;
- Onyesha uhusiano kati ya ugavi na mahitaji;
- Linganisha jamii yao ya ndani na jamii mbalimbali za dunia kulingana na wanachama, mila na desturi, huku ukieleza jinsi matukio ya ulimwengu yanayoathiri Kentucky; na
- Chunguza jinsi jamii zinavyofanya kazi pamoja.

## Mifano ya Kazi ya Mtoto Wako Shuleni::

Kutumia ramani kutafuta nchi mbalimbali;
Kueleza jinsi sifa za kitamaduni, kiuchumi na kijiografia zinavyoathiri jinsi wanadamu wanavyosonga;
Kueleza jinsi serikali za nchi mbalimbali zinavyoshughulikia matatizo yao;
Kulinganisha tamaduni na mila za watu duniani kote; na
Kueleza jinsi nchi zinazofanya biashara zinavyoathiri ulimwengu.

## Jinsi ya Kumsaidia Mtoto Wako Nyumbani::

Mtie moyo mtoto wako aulize maswali. Mtoto wako anapouliza maswali, badala ya kutoa majibu mara moja pendekeza ufikirie mahali ambapo jibu linaweza kupatikana.
Zungumza kuhusu nchi mbalimbali zinapotokea kwenye habari na kupata nchi kwenye ramani.
Linganisha maisha ya kila siku nchini Marekani na maisha ya watu katika nchi nyingine. Kwa mfano, watoto katika nchi nyingine wanakula nini kwa chakula cha mchana? Nyumba zinaonekanaje ulimwenguni kote?
Angalia habari za magazeti kutoka nchi mbalimbali zinazoripoti tukio moja. Jadili kufanana na tofauti katika makala.
Zungumza na mtoto wako kuhusu umuhimu wa ushiriki wa raia, kama vile kupiga kura, n.k., na utafute mifano ya matukio ya zamani na ya sasa.

## Maswali Unayoweza Kumuuliza Mtoto Wako:

Je, ungependa kuona au kutembelea nchi gani?
Je, ni tamaduni au mila zipi kutoka duniani kote unazoziona za kuvutia?
Je, maisha yanafananaje na yanatofautiana vipi katika jamii kote ulimwenguni?
Ni bidhaa gani (mali, vitu vinavyotumika kwa mauzo au biashara) yanayoingizwa na kusafirishwa kutoka Kentucky?

## Maswali Unayo weza Kumuuliza Mwalimu wa Mtoto Wako::

Ni nchi na maeneo gani yatasomwa mwaka mzima?
Ni vitabu au mada gani zingemsaidia mtoto wangu kufahamu utamaduni zaidi?
Je, mimi na mtoto wangu tunaweza kutembelea wapi katika jamii ili kusaidia kile kinachofundishwa darasani?

Ni nyenzo gani zinapatikana kusaidia kujifunza kuhusu ujuzi wa masomo ya kijamii?